# KENYA PRIVATE SCHOOLS ASSOCIATION

## DARASA LA 8 - Muhula wa Pili - 2022

## KISWAHILI: Sehemu ya Kwanza - Lugha

**Muda: Saa 1 Dakika 40**

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibia. Kijitabu hiki kina maswali 50.
2. Ikiwa utataka kuandika chochote ambacho si jibu andika katika kijitabu hiki.
3. Ukisha chagua jibu lako lionyeshe katika KARATASI YA MAJIBU na wala sio katika kijitabu hiki cha maswali.

**JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU**

4. Tumia penseli ya kawaida
5. Hakikisha ya kwamba yafuatayo yameandikwa katika karatasi ya majibu.

NAMBA YAKO YA MTIHANI
JINA LAKO
JINA LA SHULE YAKO

6. Kwa kujaliza visanduku vyenye namba zinazokuhusu, onyesha namba yako kamili ya mtihani (yaani namba ya shule, na zile namba tatu za mwisho za mtahiniwa) katika sehemu iliyotengwa mwanzo wa karatasi ya majibu.
7. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
8. Iweke safi karatasi yako ya majibu na usiikunje.
9. Kwa kila swali 1 - 50 umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B, C, D. Ni jibu MOJA tu kati ya hayo manne ambalo ni sahihi. Chagua jibu hilo.
10. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari kwenye kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndiyo jibu.

**Kwa Mfano:**

Katika **Kijitabu cha maswali:**

**26.** Kushika mkia ni ____________
A. kuwa wa kwanza
B. kuwa mkiani
C. kubaki na mkia
D. kuwa wa mwisho

Jibu sahihi ni D
Katika **Karatasi ya majibu:**

25. [A] [B] [C] [D]    26.[A] [B] [C] [~~D~~]    27. [A] [B] [C] [D]    28.[A] [B] [C] [D]

Katika visanduku vinavyoonyesha majibu ya maswali, swali namba 26 kisanduku chenye herufi D ndicho kilichojalizwa.

11. Jaza kisanduku chako vizuri. Kujaliza kwako kuwe kweusi kama inavyowezekana.

**Soma vifungu vifuatavyo vyenye nafasi 1 - 15. Umepewa majibu manne hapo. Chagua jibu lifaalo Zaidi kujazia pengo.**

Ghafla, upepo 1________ ulianza kuvuma kutoka mashariki. 2________ tulikokuwa tukielekea. Nilipoangalia juu niliona 3________ yakisukumwa na upepo haraka haraka. Kisha mwaso ukaanza. Radi zilipasuka zikifuatana. 4________ , matone makubwa ya mvua yakaanza kutuangukia.

Tulilazimika 5________ kibanda kibovu kilichokuwa 6________ ili 7________ . Hakikutufaa sana kwani kilikuwa kinavuja mno. Hatukuwa na la kufanya ila 8 kwani tulikuwa tumeshikwa na 9________ . Mvua ilipo 10________ ilikuwa kila mtu 11________ . Giza lilikuwa limeshaanza kuingia. NIliingia 12________ na kubadilisha nguo upesiupesi na kwanza shughuli 13________ za nyumbani. Wacha mvua iendelee kunyesha. Ilinyesha 14________ 15________ .

**1.** A. mingi B. nyingi C. kali D. mwingi

**2.** A. hapo ndipo B. hivyo ndiyo C. huko ndiko D. humu ndimo

**3.** A. wingu mzito B. mawingu mazito C. mawingu nzito D. mawingo mizito

**4.** A. sako kwa bako B. unyounyo C. bak bandika bak bandua D. punde si punde.

**5.** A. kukimbilia B. kutoroka C. kukimbia D. kuenea

**6.** A. kando mwa barabara B. juu ya barabara C. ubavuni ya barabara D. kando ya barabara

**7.** A. kujipusa B. kubari C. kujibari D. kujificha

**8.** A. kuuma vidole B. kula huu C. kujizatiti D. kujikaza kisabuni

**9.** A. ushikwapo shikamana B. moja shika si kumi nenda urudi C. tulikuwa na mshike mshike D. ilibidi tushike adabu

**10.** A. pusa B. poa C. potea D. jibari

**11.** **A.** nenda zako B. unyounyo C. mguu niponye C. ajikune ajipatapo

**12.** A. kwa nyumba B, katika nyumbani C. nyumbani D. nyumba

**13.** A. nyingine B. zingine C. ingine D. mingine

**14.** A. kudinda B. kidindia C. chepechepe D. Vurr!

**15.** A. Siku kutwa B. asubuhi na machana C. usiku kucha D. bukrata

**<u>Kwa maswali 16 - 30, chagua jibu kulingana na maagizo.</u>**

**16.** Wingi wa sentensi:

*Waraka niliousoma unahusu jambao geni kwangu.*

A. Nyaraka nilizozisoma zinahusu jambo geni kwetu
B. Nyaraka tulizozisoma zinahusu mambo mageni kwetu.
C. Waraka tuliousoma unahusu mambo mageni kwetu
D. Nyaraka tuliousoma inahusu mambo ngeni kwangu.

**17.** Chagua sentensi yenye nomino dhahania.

A. kusafiri kwake kumemfikisha mbali
B. mburukenge hutumia mkia wake mrefu kama silaha.
C. uongo hauwezi kumfikisha mtu mbali
D. Kisumu I karibu na Ziwa Viktoria.

**18.** Chagua neno lenye maana sawa na <u>mighairi ya</u>

A. mradi
B. pasipo
C. isipokuwa
D. bali

**19.** Ni gani kiwakilishi katika sentensi hii?

*Wao hucheka hadi wakalia.*

A. hucheka
B. hadi
C. wao
D. wakalia

**20.** Chagua usemi taarifa wa:

*"Kwa nini mnamwajiri mtoto mdogo?" Afisa wa maslahi ya watoto aliuliza.*

A. Afisa wa maslahi ya watoto alimwuliza kwa nini alimwajiri mtoto mdogo.
B. Afisa wa maslahi ya waotto alimwuliza kilichomfanya amwajiri mtoto mdogo.
C. Afisa wa maslahi ya watoto aliwauliza kwa nini alimwajiri mtoto mdogo.
D. Afisa wa maslahi ya watoto aliwauliza kilichowafanya wamwajiri mtoto mdogo.

**21.** Umbu, mkoi, mpwa, halati : wote ni ___

A. jamii
B. nasaba
C. mwarafiki
D. wake

**22.** Miereka ni ___

A. mchezo wa mpira mdogo wa kurusha
B. mchezo wa kupigana na kuangushana
C. mchezo wa kurukaruka
D. mchezo wa kushikana na kuangushana

**23.** Wanafunzi wetu hupata chamcha saa 6.45 adhuhuri wakati huu ni ___

A. saa kumi na mbili na dakika arobaini na tano
B. saa moja kasorobo
C. saa sita kasorobo
D. saa saba kasorobo

**24.** Kuwa na <u>mkono wa paka</u> ni

A. kuwa mzembe
B. kupenda kupigana
C. kuwa mwepesi kwa kazi za mkono
D. kuwa maskini

**25.** Chagua nomino kutokana na kitenzi <u>'nyamaa'</u>

A. nyamaza
B. kunyamavu
C. sikio
D. unyamavu

**26.** Chagua wingi wa sentensi: Hukujua kuwa ningekutembelea?

A. Hawakujua kuwa tengewatembelea.
B. Hamkujua kuwa tungewatembea?
C. Hamkujua kuwa tuengmtembelea?
D. Hamkujua kuwa ningewatembelea?

**27.** Chagua ukanusho sahihi wa:

*Mama hufika shuleni mapema*

A. Maria hafiki shuleni mapema
B. Maria huchelewa kufika shleni.
C. Maria huwa hafiki shuleni mapema
D. Maria hajafika shuleni mapema.

**28.** Viambishi 'ki' vimetumika kuonyehsa nini katika sentensi hii?

Kitanda kile **<u>ki</u>**likuwa ki**<u>ki</u>**undwa na seremala

A. masharti, wakati
B. ngeli, udogo
C. ngeli, wakati
D. kiwakilishi. namna

**29.** Mahali ambapo vitu vya kale huhifadhiwa huitwa

A. ufuo
B. maabara
C. karakana
D. makavazi

**30.** Bainisha maneno yaliyopigwa kistari kwenye sentensi ifuatayo.

*Mtoto* ***<u>mtundu aghalabu</u>*** *huadhibiwa kila mara.*

A. kielekezi, kivumishi
B. kitenzi, kiwakilishi
C. nomino, kielezi
D. kivumishi, kiunganishi.

**Soma habari ifuatayo kisha ujibu maswali 31 - 40**

Ninaikumba vyema siku hiyo. Sitaweza kuisahau kamwe aushini. Ziara hiyo iliyotumbukia nyongo **imenata kama gundi** ubongoni. Ilikuwa siku ya Sabato mnamo Septemba mwaka jana. Tulikuwa tumeifunga sagari ya kuelekea katika maonyesho ya kielimu kuhusu mimea. Ndipo methali ya siku njema huonekana asubuhi ilipokosa maana. Tulikuwa tukifikiri kuwa mambo yote yangekuwa shwari bila taksiri lakini ole wetu. Yaliyotufika siku hiyo yalikuwa ya kutia kihoro.

Tuling'oa nanga alfajiri kangaichi baada ya kumpigia dua Mkawini. Tulikuwa na furaha na bashasha si kalili kwani wengi wetu hawakuwa wamepata fursa hiyo. Kwa kweli ilikuwa **adimu shabiku kaburi la baniani.** Idadi kubwa ya wanafunzi ilikuwa ikielekeza mawazo yao kwa kujivinjari katika ziara hiyo ya kielimu. Ilikuwa nadra kuwapata wanafunzi wakijiwa na usingizi kutokana na hali ya furaha iliyozagaa basini. Mighairi ya hayo, tulikuwa tukisafiri kuelekea katika mji mkuu ambao kwa wengi, ulikuwa ruiyani tu.

Baada ya muda wa mawe kuotesha mizizi, masaibu ya siku yalianza. Puum! Mlipuko mkubwa **uliotosha kuwaamsha wafu** ulisikika huku basi nalo likisimama kwa kishindo kikubwa. Nilikuwa **nikitetemeka na kutetereka mathalan unyasi msimu wa kimbunga.** Fuadi nayo ilidunda dududu kifuani mwangu kwani woga ulinivaa na kunigubika gubigubi.

Gurudumu lilikuwa limeharibika. La shani ni kuwa, siku iyo hiyo ndiyo dereva wetu alikuwa amekosa kubeba gurudumu la spea. Mungu si Athumani. Aliyekuwa akiandamana nasi sako kwa bako; dereva wa basi hilo lingine, alikuwa nalo. Walibadilisha kwa muda wa nguchiro kunawia mater na tukashika barabara. Tuliendelea bila kasoro yoyote. Baada ya kilomita kadhaa, furaha ilisambaa tena tukawa **tumetulia tuli kama maji mtungini.**

Hata hivyo, hatukudhukuru kuwa hicho kilikuwa kionjo tu. Mambo yalikuwa bado. Basi letu lilipangiwa kujionea mengi. Joto dakika baada ya nyingine. Hali ikawa ni joto lisilokadirika wala kuelezeka. Jasho lilianza kututiririka kama maji mferejini. Gari lilisimamishwa kando ya barabara. Walifanya uchunguzi ili kumaizi kulikokuwa na shari. Tulingoja kikonzo na hatimaye idili zao zilifua dafu. Kinaya cha mambo, injini nayo ilikuwa na shida. Chelewa chelewa utapata mwana si wako. Walianza gange punde tu walipong'amua palipokuwa na doa. Walitatua shida kisha tukaendelea na safari.

Tulifika maonyeshoni tukiwa tumelimatia kuliko tulivyotarajia. Zilikuwa zimebakia saa chache maonyesho yaishe. Heri kenda shika kuliko kumi nenda. Tulijinatia tuliyoyapta na tuliyokosa tukang'amua kuwa fursa ni nyingi. Tulirudi shuleni huku tukiwa na mioyo mizito kwani tulikuwa tumeendewa mvange na mengi. Halhamdulilahi! Safari ya kurudi ilikuwa tofauti na ya kwenda. Ingawa tulifika salama salmini, ziara hiyo ilikuwa na masaibu si haba.

**31.** Msimulizi anadokeza kuwa hawezi kusahau siku husika kwa sababu ___

A. ilikuwa siku ya safari
B. ilikuwa siku ya sabato mwezi wa Septemba
C. ilikuwa siku njema
D. safari ya siku hiyo ilijaa masaibu

**32.** Ni fungu lipi la maneno lililotumiwa kwenye aya ya kwanza ambalo halionyeshi kuwa safari hii ilijaa mkosi?

A. ziara ilitumbukia nyongo
B. ziara hiyo imenata kama gunda.
C. methali ya siku njema huonekana asubuhi ilipokosa maana
D. yaliyotufika yalikuwa ya kutia kihoro.

**33.** Sentesi "*. . . tumetulia tuli kama maji mtungini*" imetumia fani zipi za lugha, mtawalia?

A. chuku, tashbihi
B. istiara, tanakali
C. tanakali, tashbihi
D. tashbihi, chuku

**34.** Wanafunzi wengi hawangesinzia kwenye safari hii kwa sababu ya:

A. safari kuwa ndefu
B. masaibu yaliyowapata
C. hali ya bashasha iliyowajaa
D. uchovu waliokuwa nao.

**35.** Inabainika kuwa kwa wale wanafunzi waliokuwa safarini

A. wengi hawakuwa wamezuru mji mkuu.
B. wote niwenyeji wa mji mkuu
C. wachache tu ndio hawakuwahi kuzuru mji mkuu
D. msimulizi pekee ndiye hakuwa amezuru mji mkuu.

**36.** Fungu la ". . . mlipuko uliotosha kuwaamsha wafu" imetumia fani gani ya lugha?

A. tashhishi
B. tashbihi
C. takriri
D. chuku

**37.** Kisa cha dereva kukosa kubeba spea ya gurundumu siku ya safari linaelezeka kwa methali

A. haba na haba kujaza kibaba
B. chururu si ndo ndo ndo
C. usipoziba ufa utajenga ukuta.
D. siku ya nyani kufa matawi yote huteleza.

**38.** Chagua fungu ambalo si tashbihi kama ilivyotumika kwenye habari hii.

A. imenata kama gundi
B. adimu shabiki kaburi la baniani.
C. muda wa nguchiro kunawia mate
D. tetemeka na tetereka mathalani unyasi msimu wa kimbunga

**39.** Safari hii ilikuwa ya kuenda:

A. maonyesho ya kilimo mjini
B. kuzuru mji mkuu
C. maonyesho ya kielimu kuhusu mimea
D. kutembelea shule iliyokuwa mjini

**40.** Kulingana na aya ya mwisho, wanafunzi waliwasili kwenye maonyesho wakiwa

A. wamesinyaa sana
B. wamechoka kupita kiasi
C. wamechelewa
D. wamefurahi sana

**Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali.**

Katika tamaduni za Kiafrika salamu au maamkizi ni muhimu sana katika jamii. Salamu ni maneno yanayotumiwa kujuliana hali kati ya mtu na mwingine au mtu na kundi. Aghalabu salamu hutegemea umri, wakati na uhusiano wa mhusika na mwenzake. Asubuhi watu huamkiana kwa kutumia maneno kama vile sabalheri na habari za asubuhi. Kuna maamkizi ya jioni, usiku na nyakati zote. Ikiwa mtu atasalimiana bila kuzingatia wakati ataonekana kama aliye na kasoro. Hii ni kwa sababu salamu ni mojawapo wa vitendo ambavyo kila mja hufunzwa na familia yake pamoja na jamii anapokuwa mtoto mdogo sana.

Salamu pia huzingatia umri. Jinsi mtoto anavyomsalimia mwalimu, mzazi wake au mtu yeyote yule aliyemzidi kwa umri ni tofauti na anavyomwamkia mtoto mwenzake. Vijana wanafaa wawasalimie wazee 'shikamoo?" nao wanajibu marahaba. Marika hutumia salamu kama vile hujambo, waambaje na u hali gani? Mtu anayezingatia umri anapoamkiana huwa anachukuliwa kuwa mnyenyekevu na mwenye heshima. Wanafunzi shuleni wanafaa kuonyesha heshima wanapowaamkia walimu na wafanyakazi mbalimbali shuleni. Watu wanapoamkiana huwa ni dalili ya utangamano na amani katika jami. Watu wanaogombana bila shaka huwa hawapatani kwa hivyo huenda wakakosa kusalimiana.

Tangu jadi watu wawili walipokosana au vikundi viwili vilipozozana na kukawa na wapatanishi, hatimaye wahusika walisalimiana kwa kushikana mikono kama ishara ya **kuzika uhasama** wao katika kaburi la sahau na kuanza maisha mapya yenye amani. Unapomwamkia mtu usiyemfahamu huwa unamwalika katika mazungumzo zaidi hasa ya kujua jina lake, anakotoka na anakoelekea na hatimaye huenda mkajenga uhusiano wa kudumu. Hebu kumbuka ulivyomwamkia mwanafunzi mgeni shuleni au darasani mwenu. Punde tu mliposalimiana ndipo mazungumzo yenu yalipong'oa nanga. Hivyo ndivyo mlivyoweza kujua kuhusu kila mmoja wenu. Pengine mshakuwa marafiki wa kufa kuzikana.

Salamu bila shaka ni mojawapo ya desturi nzuri za Waafrika. Tuboreshe uhusiano wetu katika jamii kwa kuwasalimia wenzetu na kuwajulia hali. Mtu aliye na changamoto fulani hasa huenda akatulia na kujihisi mwenye amani baada ya kusalimiwa au kujuliwa hali na watu walio karibu naye. **Hakuna chema kisicho na dosari**. Ni vyema kuwa mwangalifu. Kuna baadhi ya watu hutumia salamu kama mbinu ya kumlet karibu mtu wanayetaka kumdhuru. Wanaweza kusalimia mtu na kumteka nyara baada ya kumkaribia. Kwa sababu ya usalama wetu, ni vyema kutowasalimia watu kwa kuwashika mikono ili kujjiepusha na ugonjwa wa Korona

**41.** Ni gani kati ya maneno haya si kisawe cha salamu?

A. utweshi
B. maamkio
C. maamkizi
D. matwezo

**42.** Jinsi watu wanavyosalimiaana aghalabu haitegemei _____

A. umri
B. wakati
C. elimu ya mtu
D. uhusiano kati ya wahusika

**43.** Mtu mnyenyekevu na mwenye heshima ni yule anayezingatia nini katika maamkuzi yake?

A. umri
B. wakati
C. heshima
D. mazingira yake

**44.** KUsalimiana kwa kushikana mikono kwa waliozozana baada ya upatanisho ni dalili ya _____

A. unyenyekevu.
B. heshima
C. kuanza maisha mapya yenye amani
D. urafiki kuisha

**45.** Kusalimiana kwa kushikana mkono kuna hatari zifuatazo ila ___

A. mtu usiyemjua huenda akudhuru kwa njia yoyote ile.
B. kuna uwezekano wa kujenga urafiki na mgeni
C. uwezekano wa kutekwa nyara na watu wabaya
D. hatari ya kuambukizwa ugonjwa wa korona

**46.** Methali gani nyingine ingetumika katika aya ya nne mbali na ile iliyopigiwa mstari?

A. mtoto wa nyoka ni nyoka.
B. mbio za sakafuni huishia ukingoni.
C. hakuna masika yasiyo na mbu.
D. kikulacho ki nguoni mwako.

**47.** Sabalkheri na masalkheri ni maamkuzi ambayo yanazingatia

A. umri
B. hali
C. nyakati
D. cheo

**48.** Mtu anaonekana kuwa na kasoro iwapo

A. atapita mwenzake bila kumpa salamu
B. atamsalimia mtu bila kuzingatia umri
C. atasalimiana bila kuzingatia uhusiano uliopo kati yao.
D. atasalimiana bila kutumia neno ‘shikamoo’

**40.** Msimulizi anapotumia fungu ‘kuzika uhasama’ ametumia fani gani ya maneno

A. chuku
B. tashhisi
C. tashbihi
D. takriri

**50.** Kichwa kinachofaa zaidi makala haya ni

A. hasara za salamu
B. jinsi ya kusalimiana
C. tamaduni zetu
D. maamkizi